



**MAMLAKA YA UDHIBITI WA  
HUDUMA ZA NISHATI NA MAJI  
(EWURA)**



**TAARIFA KWA UMMA**

**(Imetolewa chini ya Kifungu cha 19 cha Sheria ya Mamlaka ya Udhhibiti wa Huduma za Nishati na Maji, Sura ya 414 ya Sheria za Tanzania)**

**TAARIFA** inatolewa kwa umma kwamba Mamlaka ya Udhhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA) imepokea maombi ya leseni ya kuzalisha umeme kutoka kwa Kampuni ya NextGen Solawazi Limited. EWURA inakaribisha maoni au pingamizi kuhusiana na maombi hayo ya leseni. Taarifa za mwombaji pamoja na aina ya leseni iliyoombwa zimetolewa hapa chini:

<b>Na.</b>	<b>MAELEZO</b>
<b>Jina na anuani ya Mwombaji</b>	NextGen Solawazi Limited, 153 Barabara ya Haile Selassie, S. L. P 79042, Dar-es-Salaam.
<b>Eneo la Mtambo</b>	Kiwanja Namba 242-255, Eneo Maalum la Kiuchumi Kigoma, Manispaa ya Ujiji, Mkoa wa Kigoma.
<b>Taarifa za Wanahisa</b>	1) Feroz Kassam, <b>33.3%</b> . Kiwanja Namba 465, Barabara ya Haile Selassie, P. O. Box 79042 Dar-es-Salaam.  2) Anil Nanji, <b>33.3%</b> . 1101 Napoli Drive, Pacific Palisades, CA 9027, USA.  3) Mayank Bhargava, <b>33.3%</b> . 2303 Colonel Lindsay Court, Falls Church, VA 22043. USA,
<b>Maelezo ya Mtambo na Matumizi</b>	Megawati 5 kwa kutumia nishati ya jua, Mtambo una paneli 16,116, inveta 158 na transfoma mbili (2) kuzalisha umeme wa msongo wa kilovoti 33 utakaounganishwa na mfumo wa usambazaji umeme wa TANESCO katika Gridi Ndogo ya Kigoma.
<b>Aina na Muda wa Leseni</b>	Leseni ya muda mrefu ya kuzalisha umeme kwa miaka ishirini (20)

Mtu yeyote mwenye maoni au pingamizi kuhusiana na maombi haya awasilishe kwa maandishi kabla ya saa 10 jioni ndani ya siku ishirini na moja (21) tangu siku ya kutolewa kwa tangazo hili. Maombi ya leseni yanaweza kuonyeshwa kwa mtu kwa maombi maalum ya maandishi.

**Imetolewa na:  
Mkurugenzi Mkuu-EWURA**